

Tangazo kwa Vyombo vya Habari

MWALIKO KWA VYOMBO VYA HABARI

Nini: Taasisi ya UONGOZI, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Uchumi Barani Afrika (UNECA), itafanya kongamano la kikanda lenye dhima “**Kuimarisha usimamizi wa madini mkakati kwa ajili ya viwanda vya kijani na maendeleo endelevu barani Afrika**”. Kongamano hili ni tukio muhimu litakalofanyika kabla ya Mkutano wa 12 wa Kikanda wa Maendeleo Endelevu, unaoratibiwa na UNECA. Kongamano litajadili masuala ya usimamizi wa madini mkakati, ikiwemo mikakati ya kiseru, uwezo na fursa; na kutoa mapendekezo ya namna ya kuongeza thamani, kuchochea viwanda vya kijani, na kuimarisha tabianchi.

Lini: 27 Aprili 2026.

Wapi: Makao Makuu ya UNECA, Addis Ababa, Ethiopia.

Nani: Mgeni rasmi wa kongamano hili atakuwa Mhe. Hailemariam Dessalegn Boshe, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia. **Wasilisho kuu litatolewa na Dkt. Paul Jourdan,** Mchambuzi Sera wa Madini anayejitegemea. Washiriki wengine ni viongozi waandamizi kutoka nchi mbalimbali barani Afrika – na sekta zote ikiwemo sekta ya umma, sekta binafsi, sekta ya elimu ya juu, na sekta ya asasi za kiraia.

Namna: Kongamano litajumuisha ufunguzi, mijadala ya jopo, mawasilisho ya kitaalamu, na mjadala wa kupaza sauti za vijana, wanawake, na jamii katika mada husika.

Lengo: Kongamano linalenga kutoa fursa ya kujadili namna ya kuhakikisha usimamizi madhubuti wa madini mkakati ili kuchochea viwanda vya kijani na maendeleo endelevu barani Afrika. Malengo mahususi ni:

- i. Kuimarisha uelewa wa usimamizi wa madini mkakati barani Afrika, ikiwemo mikakati ya kiseru, kwa kutumia mifano ya sasa na ile ya zamani.
- ii. Kuainisha namna bora ya kuchimba madini mkakati na kuimarisha mnyororo wa thamani barani Afrika ili kuchochea viwanda vya kijani na maendeleo jumuiishi; na
- iii. Kujadili na kupendekeza miongozo inayozingatia usawa baina ya uchimbaji madini na utunzaji mazingira, pamoja na maslahi na haki za jamii.

Waandishi wa habari wanaalikwa kwa ajili ya kuhudhuria tukio la ufunguzi **kuanzia saa 2:00 Asubuhi – 5:00 Asubuhi.**

AFRICA'S CRITICAL MINERALS FORUM

27 APRIL 2026
ADDIS ABABA, ETHIOPIA



HARNESSING AFRICA'S CRITICAL
MINERALS FOR GREEN INDUSTRIALISATION
AND SUSTAINABLE DEVELOPMENT

Kuhusu Taasisi ya UONGOZI: Taasisi ya Uongozi kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu Barani Afrika, maarufu kama Taasisi ya UONGOZI (*UONGOZI Institute*), ni taasisi ya kikanda ya kuimarisha kada ya uongozi iliyo chini ya Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taasisi ilianzishwa mwaka 2010 na Serikali za Tanzania na Finland kwa lengo la ya kujenga na kuimarisha viongozi wa Afrika ili kukidhi matakwa ya ndani ya kutoa huduma kwa wananchi na kuyafikia maendeleo endelevu.

Taasisi inatambua kwamba sifa za uongozi hujengwa kwa namna endelevu. Hivyo, programu katika mihimili yake miwili – uongozi na maendeleo endelevu – zinatekelezwa kupitia maeneo makuu manne: mafunzo ya uongozi, mijadala ya kisera, tafiti, na ushauri wa kitaalamu. Wateja wake ni pamoja na taasisi na watu binafsi kutoka kwenye sekta zote.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na: Suzana Aroko, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mahusiano kwa Umma, Taasisi ya UONGOZI | Barua pepe: saroko@uongozi.or.tz | www.uongozi.go.tz

Shiriki katika mjadala mtandaoni: # AfriCMF2026 #ARFSD12